# HATI YA HUDUMA

*"Tumeazimia kutoa huduma bora inayolingana na thamani ya fedha yako"*

WILDLIFE RESEARCH & TRAINING INSTITUTE
Discover Beyond

## Sisi ni kina nani

**Taasisi ya Utafiti na Mafunzo ya Wanyamapori (WRTI)** ni Shirika la Umma chini ya Idara ya Wanyamapori katika Wizara ya Utalii na Wanyamapori. Taasisi hii ilianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori nambari 47 ya mwaka wa 2013 na ikaanzishwa rasmi kupitia kwa Tangazo la Serikali nambari 4862 la tarehe 17 Julai, 2020. Majukumu halisi ya WRTI yamebainishwa katika kifungu cha 51 cha sheria hiyo, ambayo ni kuratibu na kuendesha utafiti na mafunzo kuhusu wanyamapori nchini Kenya.

## Dira Yetu

Taasisi ya kitaifa ya utafiti na mafunzo ya wanyamapori yenye uwezo wa kushindana katika ngazi za kimataifa.

## Dhamira Yetu

Kuratibu na kutekeleza utafiti na mafunzo ya wanyapori kupitia kwa ubunifu, uhamasishaji wa maarifa na teknolojia kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi endelevu wa wanyamapori.

| HUDUMA INAYOTOLEWA | MAHITAJI YA KUPOKEA HUDUMA | GHARAMA | MUDA WA HUDUMA |
|---|---|---|---|
| **HUDUMA ZA MAFUNZO** | | | |
| Usajili wa wanafunzi | Mahitaji ya mtaala ulioidhinishwa. | Kwa mujibu wa ada ya maombi iliyoidhinishwa | Siku 21 za kazi baada ya kufungwa kwa maombi |
| Ufundishaji/mafunzo | Usajili wa kozi mahudhurio darasani | Kwa mujibu wa muundo wa ada iliyoidhinishwa | Miezi 18 kozi za stashahada<br>Miezi 9 kozi za astashahada<br>Kozi za muda mfupi; kulingana na muda ulioidhinishwa |
| Mahafali | Kukamilisha mtaala na kufanikisha mtihani fomu ya mahafali iliyojazwa<br>Kukamilisha ukaguzi wa mwisho | Kwa mujibu wa ada ya mahafali iliyoidhinishwa | Siku 21 baada ya notisi ya mahafali |
| **HUDUMA ZA UKARIMU** | | | |
| Mikutano ya kitaaluma | Kuhifadhi abra kupitia kwa baruapepe tarehe na idadi ya watu walioidhinishwa agizo la ununuzi wa kawaida | Kwa mujibu wa viwango vilivyoidhinishwa | Mara moja |
| Huduma za malazi | Kuhifadhi abra kupitia kwa baruapepe, simu au kufika moja kwa moja | Kwa mujibu wa viwango vilivyoidhinishwa | Mara moja |
| Huduma za mgahawa wa taasisi | Malipo | Kwa mujibu wa bei ya vyakula iliyoidhinishwa | Mara moja |
| Shughuli za nje zinajumuisha: kukita kambi, matembezi milimani, kutazama wanyamapori, ujenzi wa umoja miongoni mwa kundi, kifungua kinywa au chajio msituni, kupanga viwanja, kuogelea, kuteleza mbadala, na kufanya pikiniki. | Kiingilio | Kwa mujibu wa viwango vya shughuli vilivyoidhinishwa | Mara moja |
| Ziara katika jumba la makumbusho | Kiingilio | Kwa mujibu wa viwango vilivyoidhinishwa | Mara moja |
| **HUDUMA ZA UTAFITI WA WANYAMAPORI** | | | |
| Leseni za utafiti wa wanyamapori | Maombi ya vibali vya utafiti kupitia mtandaoni kulingana na mwongozo ulioidhinishwa | Kwa mujibu wa viwango vya ada za vibali vilivyoidhinishwa kwa makundi mbalimbali | Ndani ya siku 90, lakini iwapo kutatokea na kuchelewa, sababu zake zitaelezwa kwa mwombaji na muda mpya wa utekelezaji utakubaliwa. |
| Huduma za ushauri wa kitaalamu | Mikataba ya ushauri iliyoidhinishwa au barua ya tuzo ya ruzuku | Kwa mujibu wa bajeti zilizoidhinishwa | Kwa mujibu wa muda wa utekelezaji wa mradi kama ulivyoidhinishwa katika mikataba au barua ya tuzo ya ruzuku |
| Itifaki ya kushirikisha taarifa za wanyamapori | Barua ya maombi au baruapepe ya pendekezoikieleza sababu za maombi, pamoja na barua rasmi kutoka kwa taasisi kwa niaba ya wanafunzi au washirika. | Bila malipo | Siku 14 |
| **HUDUMA ZA USAMBAZAJI NA UGAVI WA BIDHAA** | | | |
| Uteuzi wa awali wa wasambazaji waliohitimu | Kwa mujibu wa mahitaji yaliyoidhinishwa | Bila malipo | Siku 30 |
| Uchakataji na utoaji wa zabuni | Kwa mujibu wa vigezo vya tathmini vilivyoidhinishwa | Bila malipo | Siku 30 |
| Uuzaji au uondoaji wa mali | Kwa mujibu wa rejesta ya mali iliyoidhinishwa na sheria ya ununuzi wa umma (ppada) | Kwa mujibu wa PPADA | Siku 30 |
| **MALIPO KWA WANAODAI** | | | |
| Malipo kwa wasambazaji na watoa huduma | Hati ya mkataba<br>Maelezo ya benki na mawasiliano ombi la ununuzi<br>Ripoti ya tathmini<br>Fomu ya kupokelewa kwa bidhaa (GRN)<br>Nakala ya amri ya ununuzi (LPO)<br>Cheti cha ukaguzi na kukubaliwa kwa bidhaa<br>Ankara | Bila malipo | Ndani ya siku 30, na iwapo kutatokea na kuchelewa, sababu ya kuchelewa itaelezwa kwa msambazaji na muda mwafaka wa kukamilisha kuafikiwa. |

## Tathmini ya wateja

Tumejizatiti kushughulikia masuala ya wateja/wadau kwa weledi. Iwapo hutaridhika au ungependa kutupa pongezi, tafadhali wasilisha maoni yako kupitia kwa barua pepe, simu, au kwa kufika wewe binafsi ukitumia mawasiliano yetu.

**Wasiliana Nasi**

**Mkurugenzi/Afisa Mtendaji Mkuu**
Taasisii ya Utafiti na Mafunzo ya Wanyamapori
S.L.P 842-20117, Naivasha
Baruapepe: director@wrti.go.ke

**Nambari ya Simu**

+254 700000321
+254 797900800
+254 731919465
Baruapepe: wrti@wrti.go.ke

**The Commission on Administration of Justice**

**"Office of the Ombudsman"**
S.L.P 20414 – 00200, Nairobi
Simu: +254 (20) 270000/ 2303000 / 2603765/2441211
Baruapepe: info@ombudsman.go.ke
Nambari isiyotozwa ada: 0800 221 349

www.wrti.go.ke   WRTI_KE   WRTIKenya